

KENYA HIGH SCHOOL MOCK 2020

KISWAHILI PAPER 3

SEHEMU A : FASIHI SIMULIZI

1. lazima
(a) Miviga ni nini? (alama 2)
- (b) Eleza sifa tano za Miviga (alama 5)
- (c) Fafanua hasara tatu za miviga (alama 3)
- (d) Eleza changamoto tano ambazo mtafiti hukabiliana nazo anpokusanya data ya miviga (alama 10)

SEHEMU B:
TAMTHLIA – Kigogo (Pauline Kea)

2. Onyesha namna mwandishi alivyofanikiwa kukuza maudhui yafuatayo
- (i) Elimu (alama 10)
- (ii) Ujana (alama 10)
3. Mvunja nchi ni mwananchi 'Eleza ukweli wa kauli hii kwa kurejelea matukio katika tamthlia ya kigogo (alama 20)

SEHEMU YA C: USHAIRI

B. Moyo wanambia imba, dikteta simwimbie
Moyo Wanambia lumba, muhitaji mlumbie
Moyo wanambia chimba, maovu uyachimbue
Moyo wanambia woga, ndio mwazo wa maafa

Moyo wanambia kuwa, ila kasuku usiwe
Moyo Wanambia iwa, kunguni ila usiwe
Moyo wanambia pewa, cha mnyonge usipewe
Moyo wanambia woga, ndio mwazo wa maafa

Moyo wanambia nenda, penye dhuluma senende
Moyo Wanambia penda, mnyonyaji simpende
Moyo wanambia ponda, ateswaye simponde
Moyo wanambia woga, ndio mwazo wa maafa

Moyo wanambia tenda, lenye jamala litende
Moyo Wanambia unda, lenye faida liunde
Moyo wanambia tunda, lisilo sumu litunde
Moyo wanambia woga, ndio mwazo wa maafa

Moyo wanambia ota, kuwa mwizi usiote
Moyo Wanambia kata, marija yote ikate
Moyo wanambia teta, penye dhuluma patete
Moyo wanambia woga, ndio mwazo wa maafa

Moyo wanambia nyosha, penye na kombo panyoshe
Moyo Wanambia usha, mateso yote yaushe
Moyo wanambia isha, yenye majonzi yaishe
Moyo wanambia woga, ndio mwazo wa maafa

Moyo wanambia waza, yalopita yawazie
Moyo Wanambia kaza, mwovu njia mkazie
Moyo wanambia vuaza, lenye heri tuyazie
Moyo wanambia woga, ndio mwazo wa maafa

(Shairi la mbegu la E. Kezilahabi, 1988)

- (a) Fafanua dhamira ya mtunzi wa shairi hili (alama 2)
- (b) Ainisha bahari za ushauri huu kwa kutegemea
 (i) Mpangilio wa maneno
 (ii) Vipande vya mishororo
 (iii) Idadi ya mishororo kwa kila ubeti (alama 3)
- (c) Tambua aina moja ya urudiaji na utolee mfano (alama 2)
- (d) changua muundo wa shairi hili (alama 4)
- (e) Andika ubeti wa tano kwa lugha ya nathari (alama 4)
- (g) Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumika katika ushauri
 (i) Dikteka (alama 2)
 (ii) Kasuku

(iii) Mnyonyaji

USHAIRI

Ni mimi nizamishaye chini
 Mizizi kwenye majabali
 Kufyonza chumvi!

Ni mimi ninyunyizae maji
 Ili mimea ifumbue
 Nafasi zao hewani
 Ili miti ishike mimba kuzaa
 Matunda, nafaka, mizizi na viazi
 Ela mimi sili hata punje moja
 Nabaki mtupu!

Ni mimi tumbo kubwa,
 Nilijeshiba madini
 Ni mimi ninayechimba
 Kupakua raslimali
 Dhahabu, chuma, makaa...

ela yote yanaona
 Yatiririka kwao!
 Nabaki mtupu!
 Vyakula vyote nazalisha mimi
 Na mi' nabaki na njaa!

Nguo zote nawapa mimi
 Na mi' nabaki u tupu!

Madini yote nawapa mimi
 Na mi' nabaki kununua vyao!

Kazi zote nafanya mimi
 Wao wabaki kunila nguvu!

Wao wanajita bora
 Na mi' nabaki fukara!

(Shairi la S.A Mohamed Jicho la ndani, Longhorn Publishers 2002)

- (a) Lipatie shairi hili anwani mwafaka (alama 2)
- (b) Pafanua aina moja ya taswira katika shairi hili (alama 2)
- (c) Eleza ujumbe mkuu wa mtunzi wa shairi hili (alama 2)
- (d) Huu ni ushairi wa aina gani. Toa sababu ya jibu lako (alama 2)
- (e) Eleza toni ya ushairi (alama 2)
- (f) Mtunzi ametumia mbinu zipi kukuza ujumbe wake (alama 4)
- (g) Huku ukitolea mifano onyesha matumizi ya mistari mishata katika shairi hili (alama 2)
- (h) Onyesha u muhimu wa kinaya katika shairi hili (alama 2)
- (i) Tambua nafsi neni katika shairi hili (alama 2)

SEHEMU D:

Hadithi fupi (Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine)

- 6 Onyesha namna nafasi ya awanamke inavyosawiriwa kwa kuzingatia hadithi zifuatazo
- (a) Ndoto ya mashaka
- (b) Masharti ya kisasa
- (c) Mapenzi ya kifaurongo
- (d) Shogake dada ana ndevu

7.Ati umebakwa! nani akubake wewe? Wapi utakapobakwa mji pasiwe na mtu wa kukuombea?

- (a) Eleza muktadha wa dondoo hili (alama 4)
- (b) Eleza sifa mbili na umuhimu wa msemaji wa maneno haya (alama 4)
- (c) Jadili maudhui makuu katika dondoo hili (alama 12 (6 x 2))

SEHEMU YA E:

Choi la Heri

(alama 20)

8. Jadili ufaafu wa anwani chozi la Heri.